# SAFARI



## Somo hili linafanya kazi vipi?

Mpangilio: soma, jadili, fuata, kabidhi

- Tutasoma nakala katika somo
- Tutatua kujadili nakala na kujibu maswali
- Tutafuata kwa maombi ukweli tutakaogundua
- Tutaendelea kuwakabidhi wengine mamabo Ambayo Mungu ametukabidhi

## Kwa nini somo hili linafanya kazi?

Tunaunganisha mambo kadhaa yenye nguvu kwa ukuaji katika Kristo.

- **Uhusiano:** tunatazamia kuelewa uhusiano wa ukristo. Lolote ambalo Mungu ananuia kutenda katika au kupitia maisha yako, atayatekeleza kutokana na uhusiano wako naye.

- **Ufuasi:** yesu aliamuru kanisa lake kufanya wafuasi. Wafuasi hukua wakati waumini wanamfuata Kristo kwa kumpenda Mungu, kuungana na waumini, kuitumikia ulimwengu na kuikabidhi injili. Utaongozwa kupitia mfumo wa Agano Jipya wa ufuasi.

- **Unyoofu:** somo hili lina nyoosha mambo ya ukristo kuwa ya kueleweka, yenye mtazamo na safari ya kubadilisha maisha.

- **Jamii/ mafunzo:** unaweza kupata ujumbe pamoja na kundi la waumini na upokee mafunzo. Hii inakuwezesha kupata kujua waumini wengine, kuuliza maswali na kupata uzoefu.

- **Maombi:** utahimizwa kupitia ujumbe huu kwa maombi n akumtegenmea Mungu. Ukuaji wa kiroho sio matekoe ya chochote unachomfanyia Mungu; ukuaji wa kiroho ni matokeo ya mambo ambayo Mungu anatenda kupitia kwako. Tunapoomba na kumtegemea Mung, anaishi kupitia sisi.

## Je, wazo kuu ni lipi?

Miaka kadhaa iliyopita, niliwanunulia mabinti zangu hema. Kulikuwa na fito 12 fupi, fito 14 ndefu, vyuma 21 vya kuunganisha , gunia yenye rangi ya kupendeza, mkoba mdogo wa kuweka, na HAIKUWA NA MAELEZO YA JINSI YA KUUNGANISHA. Niliweka vijisehemu mbele yangu, niliona picha kwenye sanduku, lakini sikuwa na ujuzi wa kuunganisha. Niliunganisha na kung'oa fito hizo. Nikageuza, kukunja na kupinda na kulazimisha visehemu hivyo pamoja. Niliunganisha visehemu pamoja nikiwa na matumaini kwamba hatimaye nitakuwa na kitu kinachofanana na hema. Mwishowe, baada ya zaidi saa moja, hema hiyo iliweza kuunganishwa. Ilikuwa ni jambo la kusikitisha.

Habari hiyo inaelezea jinsi watu wengi wanakabiliana na ukristo. Wanapofungua "sanduku la Ukristo" limejawa na mambo kama Mungu, Biblia, Yesu, maombi, kanisa,kuhubiri, kuabudu, ubatizo, kutumikia, kutoa, vikundi vidogo, wakati mtulivu, umishonari na HAKUNA MAAGIZO MAALUM YA KUUNGANA PAMAOJA.

<u>Mpango wa Mungu wa kuungana pamoja kunahusu sehemu tatu maalum: Roho wake, Neno lake na Watu wake</u>. Kupitia Roho wake, anabadilisha tabia yetu, anatuongoza katika ukweli na anatupa nguvu kuishi kwa haki. Kupitia Neno lake, anashiriki ukweli, anaipa changamoto dhambi, anadhihirisha tabia yake, na anatuwezesha kuelewa mpango wake kwa maisha yasiyokuwa na mwisho. Kupitia watu wake, tunafunzwa kuwa wafuasi wa Kristo, tunapewa moyo na changamoto katika kutembea na Mungu, na tunaungana kwa nia njema katika ulimwengu.

<u>Lengo la mwongozo huu ni kotoa ratiba ya ufuasi wa kikristo</u>. Mwongozo hautajibu maswali yote kuhusu Mungu, Biblia, maisha ya ukristo, au maisha ya milele. Hiyo sio lengo. Mwongozo hauta jadili kuhusu mambo yote katika kijitabu. Lengo ni kutoa sehemu ya mwanzo wa mjadala na kuelewa taswira kuu. Unapoelewa lengo, kusudi za Mungu, na matarajio, mambo maalum na ukweli- inakupa maono yanayohitajika kwa ukuaji katika kristo.

## Nitatumiaje Mwongozo huu?

Mwongozo huu unatumika vyema katika muktadha wa ufuasi wa moja kwa moja au ufuasi wa kikundi kidogo. Ujumbe umeandikwa kwa njia ya pointi na maelezo mafupi. Kuna ujumbe unaotosha kushughulikia somo hili, ila tu haujaandikwa kwa kina. Hivyo basi inatoa nafasi ya kujadili.

Mwongozo huu pia uliandikiwa watu wanaotaka kufanya wafuasi wanapoendelea. Kupata muda wa kufanya wafuasi kuneweza kuwa ngumu kulingana na ratiba za maisha, wikendi zilizojawa na shughuli mingi au mikutano ya jioni. Mwongozo huu uliandikwa kwa njia ambayo inakuwezesha kuwa na mkutano (mfano wakati wa chakula cha mchana, kahawa au vikundi vidogo) na kuweza kukabidhi ukweli na imani kwa wengine.

## Ni mambo yapi yatashughulikiwa?

**Sehemu ya 1:** injili ni nini?
**Sehemu ya 2:** ni nini umuhimu wa ukristo?
**Sehemu ya 3:** ni nini malengo kuu ya ukristo?
**Sehemu ya 4:** kwa nini tunapaswa kushiriki wakati pamoja na Mungu?
**Sehemu ya 5:** ni kwa nini maandiko ni muhimu?
**Sehemu ya 6:** ninapaswa kujua nini kuhusu maombi?
**Sehemu ya 7:** mfuasi ni nani?
**Sehemu ya 8:** ina maana gani kumfuta Kristo?
**Sehemu ya 9:** wafuasi hukuzwa vipi?
**Sehemu ya 10:** wewe ni nani?
**Sehemu ya 11:** tunatembea vipi kama wafuasi?
**Sehemu ya 12:** ni kwa nini kanisa ni muhimu?
**Sehemu ya 13:** ufalme wa Mungu ni nini?
**Sehemu ya 14:** ninapaswa kufanya nini na mambo niliyojifunza?

## Ninahitajika kuleta nini?

ikiwa ungependa kuandika chini, leta Biblia yako. Baadhi ya kurasa zitaandikwa katika mwongozo. Ikipata fursa ya kuweka Biblia katika simu yako ya kidijitali, hiyo itakusaidia. Kila mmoja ataweza kupokea nakala ya mwongozo wa ufuasi. Shikilia nakala yako.

## Ni nani yuko katika kundi?

| Jina | Nambari ya Simu | Barua Pepe |
|---|---|---|
| ______________ | ______________ | ______________ |
| ______________ | ______________ | ______________ |
| ______________ | ______________ | ______________ |
| ______________ | ______________ | ______________ |
| ______________ | ______________ | ______________ |
| ______________ | ______________ | ______________ |
| ______________ | ______________ | ______________ |
| ______________ | ______________ | ______________ |

# SEHEMU YA 1: *Injili Ni Nini?*

## *Wazo kuu:*

**Injili ni habari njema ya Mungu ambayo inaokoa na kumsafisha mtu. Huwezi kukua zaidi ya injili.**

Injili ni habari njema ya Mungu kwa wanadamu. Katika injili, tunatambua kusudi letu, shida za wanadamu, tabia za Mungu, na mengi zaidi. Injili ina pointi kadhaa muhimu.

- **Mimi na wewe tuliumbwa kwa uhusiano pamoja na Mungu**.

  Mwanzo 2-3 inatueleza kwamba Adamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu na uwezo kwa uhusiano na Mungu. Hadithi hiyo inadhihirisha maongezi, muungano, na uhusiano kati aya Adamu na Mungu.

  Shauku ya Mungu ya uhusiano haikukomea kwake Adamu. Aliingia katika uhusiano wa Agano na Israeli. "*na pia nitatembea kati yenu na kuwa Mungu wenu, nanyi mtakuwa watu wangu*" (mambo ya walawi 26:12) yesu alisisitiza umuhimu wa uhusiano kwa kuwashurutisha wafuasi wake kukaa ndani yake. (Yohana 15:1-10), na kuahidi kujidhihirisha kwa wale watakao mpenda (Yohana 14:21), na kuwaashiria wafuasi wake kama marafiki. (yohana 15:15) maandiko haya yote yanaonyesha shauku ya Mungu ya uusiano.

- **Dhambi zetu zilitutenga kutokana na uhusiano**.

  Dhambi ni kuvunja amri za Mungu, na sisi sote tumetenda. "*maana wote wametenda dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu*" (Warumi 3:23) warumi 6:23 inatueleza kuhusu adhabu ya kuvunja amri za Mungu. "*Mshahara wa dhambi ni mauti*" mshahara ni kile tunapokea kwa mambo tuliyotenda. Kulingana na Biblia, sisi sote tumepokea kifo.

  Biblia inapoongea kuhusu kifo, inaongea haswa kuhusu utengano. Tunapokufa kimwili, roho zeru zinetenganishwa n amiili yetu. Tulipokufa kiroho kwa sababu ya dhambi, roho zetu zilitenganishwa na Roho wa Mungu. "na dhambi zenu zimeleta utengano kati yenu na Mungu wenu…" (Isaiah 59:2)

- **Hakuna lolote tunaloweza kufanya ili kurejesha uhusiano huu sisi wenyewe**.

  Watu wengi wanaamini kuwa matendo mema yatawapa haki na Mungu. kwa bahati mbaya, hakuna maki ya "uzuri unaotosha". Biblia haisemi, "ikiwa wewe ni mtu mwema, unakubalika mbele za Mungu" au " matendo matatu mema yatazidi tendo moja mbaya" bila kipimo chochote, je wema ni wema utoshao ni upi?

  Biblia inatusaidia kuona kwamba tatizo letu sio okosefu wa wema; tatizo ni athari za dhambi. Hatungeweza kurejesha uhusiano na Mungu kwa maana dhambi inaleta mauti na udanganyifu. Waefeso 2:1 inafunza kwamba bila Mungu kuingilia kati, tumepofushwa kwa ukweli na miungu wa ulimwengu huu. Hatuwezi fanya jambo lolote ili kumrejelea Mungu kwa maana wafu hawawezi tenda chochote; na watu waliodanganywa hawaamini.

- **Yesu alikufa msalabani ili kulipa gharama ya dhambi zetu**.

  Mshahara wa dhambi ulikuwa ni mauti. Yesu aikufa msalabani ili kulipa gharama ya dhambi zetu. Dhabihu yake iliwezesha upatanisho. "*ili kwamba tulipokuwa maadui tulipatanishwa naye Mungu kupitia kifo cha mwanawe, na zaidi, na baada ya upatanisho, tutaokolewa kutipia maisha yake*" (warumi 5:10).

- **Yesu alifufuka kutoka kwa wafu ili tupate uzima wa milele**.

  Ingawa kifo cha Yesu kililipa gharama ya dhambi zetu, ni ufufuo wake unaoleta matumaini kwa uzima wa milele. "abarikiwe Mungu na Baba... ambaye kupitia rehema zake kuu tumepata wokovu katika tumaini kupitia kufufuka kwa Yesu Kristo kutoka kwa wafu." (1 petero 1:3)

- **Yesu anatoa uzima wa milele (au uhusiamo wa upatanisho) kwa watakaotubu dhambi zao kwa kuwek aimani imani katika Yesu Kristo**.

  Yesu aliongea sana kuhusu uzima wa milele. (yohana 3:15-16; 4:14; 5:39; 6:40). Watu wengi wanapuuza kuwa uzima wa milele ni kwenda mbinguni unapofariki. Lakini Yesu hakusema hivyo. Katika Yohana 17:3, Yesu alisema "*huu ni uzima wa milele, kwamba waweze kujua...*" uzima wa milele ni kumjua Mungu. Uziam wa milele ni kupata uhusiano a upatanisho na Mungu.

  Kulingana na Biblia, uzima wa milele unapewa kwa kwa wale watageuka kutoka kwenye dhambi zao kwa kuweka imani katika mambo ambayo yesu amewatendea. Biblia inaelezea tendo la kugeuka kutoka kwenye dhambi kama kutubu. Haimaanishi kuwa mtu hatakuwa na dhambi. Inamaanisha walikuwa na shauku ya Mungu zaidi ya matendo ya dhambi. Toba ilikuwa katika ujumbe wa kwanza wa Yesu. "*tubuni, maana ufalme wa Mungu waja*" (Mathayo 4:17)

Ukweli huu sio tu muhimu kwa wokovu, ni muhimu kwa kuishi kama walio okolewa. Mambo yote maalum na mafunzo makuu ya imani yanapatikana katika ujumbe wa ijnili. Tafakari kuhusu maneno haya...

| | | | |
|---|---|---|---|
| Wokovu | Neema | upendo | msamaha |
| uchaguzi | urejesho | tumaini | uzima |
| ufalme | jamii | imani | mapenzi ya Mungu |
| jehanamu | amani | kiburi | kumtegemea Mungu |
| yesu | Messiah | furaha | Mbinguni |
| dhibitisho | Mungu | uvumilivu | Maombi |
| Enzi | Dhambi | Majaaliwa | watakatifu |

Kila neno lililotajwa na mengine mengi lina uhusiano na ujumbe wa injili. Kwa maneno mengine, jinsi unavyojua na kuelewa injili, ndivyo unavyoelewa mafunzo haya.

**Wakristo hukua ndani ya injili—sio nje ya injili.**
**Huwezi kukua kuzidi upeo wa injili.**

# SEHEMU YA 2: *Ni Nini Umuhimu Wa Ukristo?*

## *Wazo kuu:*
### Ukristo unahusu uhusiano.

**Mkristo mwema hutokana na nini?** (Andika mawazo kadhaa)

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

Kutakuwa na tofauti kadhaa kulingana na unayeongea naye, lakini watu wengi huchukulia mkristo mwema kama mtu anayeomba, kwenda kanisani, kusoma Biblia, anayetoa mali yake, kuwatumikia wengine na kuishi maisha mema. Ingawaje mambo hayo yote yanapendeza, hayawezi kumtambua mtu kama mkristo (au mkuu). Mambo yote yaliyotajwa yanaweza kutendwa na asiye mkristo. Asiye mkristo anaweza kuomba, kwenda kanisani, soma Biblia, kutoa mali yake, kuwatumikia wengine na kuishi maisha mema.

Ukristo unaaanza na INJILI YA Yesu Kristo, na Injili inahusu uhusiano.

Injili ni nini? Injili ni Habari njema ya Mungu inayookoa na kumsafisha mtu. Ni hadithi ya urejesho inayoanza katika shamba la Edeni na kuendelea hadi maisha ya milele. Tayari tumeshughulikia Injili kwa undani, tambua jinsi uhusiano unasisitizwa.

- Ubinadamu uliumbwa kwa <u>Uhusiano</u> na Mungu
- Dhambi zetu zilitutenga na <u>uhusiano</u>
- hakuna jambo tunaloweza kufanya ili kurejesha <u>uhusiano</u> huu sisi wenyewe
- Yesu alikufa msalabani ili kulipa gharama ya dhambi zetu
- Yesu alifufuka kutoka kwa wafu ili tupate uzima wa milele
- Yesu anatoa uzima wa milele (au uhusiamo wa upatanisho) kwa watakaotubu dhambi zao kwa kuweka imani imani katika Yesu Kristo.

Yesu aliongea sana kuhusu uzima wa milele. Katika Yohana 17:3. Yesu alielezea uzima wa Milele. "*Huu ni uzima wa milele. Kwamba waweze kukujua, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo ambaye umemtuma.*" **Uzima wa milele ni kumjua Mungu.** Kumjua mtu ndio umuhimu wa uhusiano. Mpango wa Mungu sio kukufanya upya; mpango wake ni kukuleta katika uhusiano unaofaa pamoja naye, na kukufanya kufanana naye Kristo. (Warumi 8:29).

Uhusiano unaanza wakati mtu anakua katika uhusiano unaofaa na Mungu. Baada ya uhusiano kuwekwa, Kristo anatuongoza katika uhusiano mbili muhimu: uhusiano na kanisa na uhusiano na ulimwengu.

<u>Je, Yesu aliwezaje kufinyanga maisha yake katika uhusiano hizi tatu</u>? Aliishi katika...

**1. Uhusiano naye Mungu Baba**

Yesu aliishi daima katika uhusiano na Mungu Baba. Alikuwa na tabia ya kujitenga pembeni/mahali kimya ili kuomba kwake Baba. Luka 6:12 inasema, "ikawa siku zile aliondoka akaenda milimani ili kuomba, akakesha usiku kucha ili kumwomba Mungu" Luke 5:16 inasema, "*lakini yeye alikua akijiepua, akaenda mahali pasipokuwa watu, akaomba*" maandika ya ziada ni: mariko 1:35, Mariko 5:45-46 na Mariko 14:32-34

Yesu alifunza kuhu kumpenda Mungu kwa kina. Katika Mathayo 22:37-38, Yesu alisema "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza"

Maisha yote ya Yesu yalielekezwa na Mungu Baba. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba hakuja , kuongea, au kutenda kwa nguvu zake. Badala yake, alielekezwa na mapenzi ya Mungu Baba. Yohana 8:42 inasema, "*...sikuja kwa nafsi yangu, bali yeye ndiye aliyenituma*" yohana 5:30 inasema "mimi siwezi kufanya neno mwenyewe, kama nisikiavyo, ndivyo nihukumuvyo, na hukumu yangu ni ya haki kwa sababu siyatafuti mapenzi yangu mimi, bali mapenzi yake aliyenipeleka." Yohana 8:28, "mimi sitendi kwa nafsi yangu, bali nina nena mambo ambayo Baba amenifunza."

Yesu alishiriki wakati peke yake pamoja na Baba. Aliwafunza wengine kuhusua kumpenda Baba kwa kina. Aliishi kulingana na mapenzi ya Baba na sio yake. Na hayo yote yaliathiri aliyotenda, aliyosema, na alipoenda. Yesu alifinyanga maisha Ambayo yanaishiwa katika uhusiano na Mungu.

**2. Uhusiano na kanisa (au wafuasi wake)**

Yesu aliishi katilka uhusiano na waumini wengine (ambao wangekuwa kanisa) alizungumza na halaiki kubwa amabo walikuwa na shauku ya mafunzo yake. Mathayo 5:1-2 inasema "naye alipowaona makutano, alipanda milimani na alipokwisjh akuketi, wanafunzi wake walimjia, akafungua kinywa chake akawafundisha..."

Yesu aliita pamoja kikundi kiogo cha watu (wanfunzi 12) kuwafunza na kuwatuma nje. Mariko 3:14 inasema "akaweka watu kumi na wawili, wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri." popote alipoenda Yesu, wanafunzi walikuwa naye. Walihudumu pamoja, walikula pamoja, wakatumikia pamoja, na wakakaa pamoja.

Yesu alishiriki muda wake mwingi pamoja na wanafunzi wake watatu: Petero, yakobo na Yohana. Watatu hawa wanaonekana pamoja na kristo katika tukio tatu kuu: Kubadilika (Mathayo 17:1; Mariko 9:2; Luka 9:28) shamba la Gethsemane na kufufuliwa kwa bintiye Jairus (Mariko 5:37; Luka 8:51)

Katika Yohana 13:35, wanafunzi wake watajulikana kwa upendo wao kwa kila mmoja. Kulingana na utangamano wake na makundi makubwa, wale 12 na wa ndani 3, utaona jinsi aliishi katika jamii na waumini. Alifunza na kufinyanga uhusiano wake wa pili.

**3. Uhusiano na ulimwengu**

Yesu aliishi katika uhusiano na ulimwengu (wale ambao hawajapatanishwa kwa Mungu kupitia Kristo). Katika matamshi yake ya kihuduma, yesu alisema kwamba "hakuja kuwaita walio na haki, bali wenye dhambi ili wakatubu." (Luka 5:27-32) kulikuwa na mtazamio mkuu wa kuwafikia wenye dhambi. Mathayo 9:10 inarekodi tukio ambalo Yesu alishiriki chakula pamoja na wenye dhambi. "basi ikawa kwamba Yesu alipokuwa kwenye meza, ndipo wakusanyaji ushuru wengi na wenye dhambi walikuja mezani na kushiriki pamoja naye na wanafunzi wake."

Yesu alikutana na mwanamke katika kisima (Yohana 4:7-42) yesu alimtetea mwanamke aliyepatikana katika tendo la uzinzi. (Yohana 8:1-11). Yesu aliienda nje ya njia zake na kushiriki mlo naye Zakayo (mwenye dhambi sugu) (Luka 19:7) yesu hakukerwa n awenye dhambi, badala yake, alikuwa na huruma.

Yesu aliishi maisha ya uhusiano pamoja naye Mungu.

Ukiweka pamoja, ukristo unahusu uhusiano. Kiini cha injili ni kwamba Mungu alikufuata kwa ajili ya uhusiano. Unapokua katika uhusiano unaofaa na Mungu kupitia Yesu Kristo, Yesu anaishi katika uhusiano kupitia kwako. Ukristo unaishiwa katika muktadha wa uhusiano tatu kuu: uhusiano wetu na Mungu, uhusiano wetu an kanisa, na uhusiano wetu an ulimwengu.

**Wazo Kuu Zaidi:** chochote ambacho Mungu ana shauku ya kutenda katika maisha yako, atatimiza kutokana na kuzidi kwa uhusiano wako pamoja naye. (ukweli huu utaonekana tunapoendelea katika somo hili.)

**Ukristo Unahusu Uhusiano.**

# SEHEMU YA 3: *Ni Nini Malengo Kuu Ya Ukristo?*

## *Wazo kuu:*

**Malengo kuu ni kumjua Mungu (kwa kushiriki wakati pamoja naye) na ili Mungu aishi Maisha yake kupitia wewe.**

**Muhtasari:**

✦ **Injili ni habari njema ya Mungu ambayo unaokoa na kumsafisha mtu. Huwezi kukua kuzidi injili.**
Uliumbwa kwa ajili ya uhusiano. Dhambi ilitenga uhusiano huo. Hakuna jambo ambalo ungeweza kufanya ili kupatanisha uhusiano huo. Yesu alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu; yesu alifufuka kutoka kwa wafu ili tupate uzima wa milele. Yesu anatoa uzima wa milele (au uhusiano wa upatanisho) kwa watakaotubu dhambi kwa kuweka imani yao katika Yesu Kristo.

✦ **Ukristo unahusu uhusiano.**
Kuna uhusinao tatu kuu: uhusiano na Mungu, Kanisa na Ulimwengu. Chochote ambacho Mungu ana shauku ya kutenda katika maisha yako, atatimiza kutokana na kuzidi kwa uhusiano wako pamoja naye.

**KUNA MALENGO MAWILI KUU KWA MAISHA YA UKRISTO:**
**1. Kumjua Mungu**
**2. 2. Ili kwamba Mungu aishi maisha yake kupitia wewe**

Baada ya kuelewa malengo kuu, tunaweza kuona mkondo wa maisha yetu. Malengo huweka mwelekeo.

**Lengo KUU ni kumjua Mungu (kwa kushiriki muda pamoja na Mungu).**

Zawadi ya Mungu kwa wanaamu kupitia yesu Kristo ni uzima wa milele (warumi 6:23). Uzima wa milele ni kumjua Mungu. (Yohana 17:3).

### Tunapata Kumjua Mungu Vipi?

- Lazima Mungu ajidhihirishe (ufunuo)
- Lazima tuamini anacho dhihirisha (imani)
- Lazima tushiriki wakati pamoja yaliyodhihirika (uhusiano)

Wacha tujadili kila sehemu ya kupata kumjua Mungu.

### Mungu amejidhihirisha vipi?

Mungu amejidhihirisha kupitia...
- Uumbaji (zaburi 19:1-4; warumi 1:20)
- Dhamiri (warumi 2:14-15)
- Kristo (Yohana 1:1, 5:18, 8:58; 14:9, 21; waebrania 1:1-2 )
- Kanuni za maandiko (Yohana 20:31; 2Timotheo 3:16; 2petero 1:21)

### Ina maana gani kuamini yale ambayo amefhihirisha?

Kwanza, maandiko yanaongea kuhusu kuokoa imani. Tunaanaza kwa kuweka imani katika ujumbe wa injili. Maandiko yanafunza kwamba kuokoa imani kuna mambo matatu: ujuzi, kibali na idhini. Ujuzi unahusu kuelewa ukweli wa biblia kuhusu injili. Kibali inakubaliana kuwa mambo hayo ni ya kweli. Idhini hutenda juua ya hayo mawili kwa kumweka kristo kama tumaini la pekee la wokovu. Katika ujuzi, ninaelewa, katika kibali, ninakubali; katika idhini , ninatenda.

Pili, maandiko yanaongea pia kuhusu kuamini yale ambayo Mungu ametamka. Ingawaje safari yetu na Mungu inaanza kwa kuokoa imani , inaendelea katika kuishi imani. Kuamini kunatenda kazi kulingana na yaliy¬o kubaika.

Tafakari jinsi ambavyo Mungu anajidhihirisha katika maandiko. Biblia inatueleza kwamba Mungu ni mtakatifu, mwenye upendo, mwenye haki, mwenye uruma, mwenye enzi, anapatikana, na ana ujuzi wote. Ni jambo moja kukubalian na mambo hayo; ni jambo linguine kuamini enzi ya Mungu wakati maisha yako yanakandamizwa, au kuamini Mungu ana upendo wakati majaribu yaja, au kujua kwamba yupo wakati unahisi upweke.

Kuamini yale ambayo Mung amedhihirisha ni kuishi kwa imani katika yale alisema katika maandiko. Ni zaidi ya ujuzi wa kiakili; inaathiri jinsi tunavyoishi. Hiyo inatupeleka katika sehemu ya tatu ya kumjua Mungu. Lazima tushiriki wakati pamoja na yaliyodhihirishwa.

## Ni jinsi gani ninaweza kushiriki wakati pamoja na Mungu?

Njia ya kipekee ya kuweza kumjua mtu ni kwa kushiriki wakati pamoja na mtu huyo. Unaweza kujua kuhusu mtu kupitia kitabu, lakini unaweza tu kumjua mtu huyo kwa kushiriki wakati pamoja naye.

**Mfano:** sababu ya uchumba ni ili kuweza kumjua mtu. Katika kuchumbiana, unaenda wanapoenda, unatenda wanachotenda; unajaribu kuelewa moyo wao, tabia zao, ndoto na mipango yao. Kwa kushiriki wakati na mtu huyo, unapata kumjua.

## Unawezaje kushiriki wakati na Mungu (na uweze kumjua)?

- Soma Biblia (Biblia ni ufunuo wa Mungu kumhusu yeye.unapata kumjua anavyo jidhihirisha katika maandiko)
- Maombi (maombi ni mazungumzo pamoja na Mungu.)
    - Ongea na Mungu katika maombi
    - Sikiza Mungu katika Maombi
- Abudu Mungu(ibada ni wakati ulio na mtazamo katika Mungu, kumshukuru kwa yale ametenda, na kujifunza zaidi kumhusu)
- Sikiza mafunzo na mahubiri ya kibiblia
- **KATIKA MAMBO HAYA YOTE, TUNAPATA KUMJUA MUNGU <u>WAKATI MTAZAMO WETU UKO KWAKE</u>**. Hatusomi tu Biblia ili tupate ujumbe; tunasoma Biblia ili kumjua. Hatuendi tu kanisani kwa sababu tunastahili; tunaenda kanisani ili kumjua. Hatuombi tu ili kumwambia Mungu mahitaji yetu; tunaomba ili tujue moyo wake katika mambo tunayopitia. <u>Tunapata kumjua Mungu kwa kushiriki wakati pamoja naye amabpo mtazamo wetu uko kwake</u>.

kushiriki wakati pamoja naye amabpo mtazamo wetu uko kwake.
Tunaposhitiki wakati na Mungu (kupata kumjua Mungu), anaishi maisha yake kupitia sisi. Ukristo sio wewe kumuishia Mungu; Ukristo ni Mungu kuishi maisha yake kupitia wewe. Ili Mungu aishi vyema kupitia wewe, ni lazima upate kumjua (kwa kushiriki muda wako pamoja naye) na ujipe katika mpango wake.

Unavyomjua Mungu zaidi, Moyo wake, Ndoto zake, shauku zake, kazi yake, ufalme wake, tabua yake- ndivyo utakavyoona jinsi anataka kuishi kupitia wewe katika wakati huo. Matendo yetu yanatiririka kutoka kwa uhusiano wetu wa upendo na Mungu.

**Malengo Muhimu Ni Kumjua Mungu (Kwa Kushiriki Wakati Na Mungu) Na Ili Mungu Aishi Maisha Yake Kupitia Kwako.**

# *Wazo Kuu:*

## Kushiriki wakati na Mungu kunapaswa kutiwa motisha na upendo.

**Mukhtasari:**

✦ **Injili ni habari njema ya Mungu ambayo unaokoa na kumsafisha mtu. Huwezi kukua kuzidi injili.**

✦ **Ukristo unahusu uhusiano.**
Kuna uhusinao tatu kuu: uhusiano na Mungu, Kanisa na Ulimwengu. Chochote ambacho Mungu ana shauku ya kutenda katika maisha yako, atatimiza kutokana na kuzidi kwa uhusiano wako pamoja naye.

✦ **Malengo kuu ni kumjua Mungu (kwa kushiriki wakati pamoja naye) na ili Mungu aweze kuishi maisha yake kupitia kwako.**

**Ni nini kinakupa motisha kushiriki wakati pamoja na Mungu?** (andika mawazo kadhaa)

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

Wakati wakristo wanaoea kuhusu kushiriki wakati pamoja na Mungu, huwa inahusiana na Biblia, maombi, au ibada. Unapowauliza watu kwa nini wao husoma BIblia, kuomba, au kuabudu-utasikia mojawapo au zaidi ya majaibu haya:

- Shauku ya ujuzi(wanataka kujua zaidi)
- Shauku ya faraja (wanataka kuhisi ubora zaidi)
- Shauku ya maombi yaliyojibiwa(wanataka Mungu aingilie kati)
- Msukumo kutokana na kanisa (waliambiwa kuwa wanapaswa)
- Utiiifu kwa Mungu (Mungu anaamuru)
- Kuhisi kuwa na hatia (wanaamini wanapaswa)
- Nidhamu (ni jambo njema kutenda)
- Uzoefu (wamekua wakitenda)

Kuna ukweli mwingi katika taarifa ifuatayo. **Sababu ya sisi kutenda tunayotenda ina umuhimu sawa na tunachotenda. Motisha yetu ndio inayotoa tafauti.**

**Kielelezo:** mume anamletea mkewe maua. Naye anafurahi sana kwa shukrani na kusema, "maua haya yanapendeza. Ni tukio lipi?"

Je, mkewe bado angejawa na furaha ikiwa mumewe angesema…

- "ni jaribio tu, nilitaka tu kuona jinsi utakavyo simulia uso wako ili nijue ni nini hukufurahisha"
- "hii haikuhusu, nilitaka tu kuhisi bora zaidi"
- "Ninakupa kitu kwa sababu nitahitaji kitu baadaye"
- "baadhi wa wanaume wenzangu kazina waliwapi wake zao maua. Sikutaka kushiriki lakini nilihisi msukumo wa kufanya hivyo"
- "uliniambia nikuletee maua, ndio hayo!"
- "nilihisi kuwa na hatia kuhusu kutokuletea maua kwa muda mrefu.natumai hii itafanya hisia hizo kupotea"
- "Nilisoma katika kitabu kwamba waume wanapaswa kufanya mabo kama haya. Ninajaribu tu kuwa na nidhamu"
- "ni tabia ambayo ninajaribu kuzoea"

Ikiwa mume angetoa yoyote kati ya majibu haya, mkewe hangefurahishwa. Kwa nini? Anataka mumewe amletee maua kwa sababu anampenda. Hataki mumewe ahisi kuwa nasukumwa au kulazimishwa kutenda. Anatakamatendo ya mumewe kutiwa motisha na upendo na shauku ya kutaka kumbariki.

Hiyo ni sawa na kushiriki wakati pamoja na Mungu. Hakuna jambo mbaya na kutaka kujua zaidi kuhusu Biblia au kumwomba Mungu ajibu maombi yako. Hata hivyo wakati sababu yetu kuu ya kusoma Biblia na kuomba inatokana na tunachoweza kupata badala ya tuliye naye- kuna jambo mbaya. Tunapaswa kushiriki wakati pamoja na Mungu kwa sababu tunampenda, tunataka kuwa naye, na tunataka kumjua zaidi.

## Sababu ya sisi kutenda tunayotenda ina umuhimu sawa na tunachotenda

Ikiwa hatutendi kutokana na upendo wa Mungu, tunapitia tu mambo ya dini. Tunaweza kuwa tunatenda mambo yaliyo sawa, lakini motisha yetu ni mbaya.

Unaposhiriki wakati naye Mungu, tafakari kuhusu nia yako. Je, uko hapo kwa sababu unampenda, au uko hapo ili kupata kitu kutoka kwake?

**Vichwa vya mjadala:**

1. Je, motisha yako ya kushiriki wakati pamoja na Mungu ina husiana vipi na lengo lako la jumla la ukristo?

2. Je, umewahi kuwa na rafiki ambaye alikaa karibu nawe ili tu kupata kitu kutok a kwako? Je, unaeza kutumia maneno yapi kuelezea uhusiano huo?

## *Wazo kuu:*

### Maandiko Ni mamlaka ya mwisho Kwa imani zote, mapito na matendo.

**Mukhtasari:**

✦ **Injili ni habari njema ya Mungu ambayo unaokoa na kumsafisha mtu. Huwezi kukua kuzidi injili.**

✦ **Ukristo unahusu uhusiano.**
Kuna uhusinao tatu kuu: uhusiano na Mungu, Kanisa na Ulimwengu. Chochote ambacho Mungu ana shauku ya kutenda katika maisha yako, atatimiza kutokana na kuzidi kwa uhusiano wako pamoja naye.

✦ **lengo kuu ni kumjua Mungu kwa kushiriki muda pamoja na Mungu.**

✦ **Kushiriki wakati na Mungu kunapaswa kutiwa motisha na upendo.**
Sababu ya sisi kutenda tunachotenda ina umuhimu sawa na tunachotenda.

**Ujumbe muhimu kuhusu Biblia:**
Biblia ni ufunuo wa Mungu kuhusu yeye. Iliandikwa na wanadamu kupitia Roho mtakatifu. Ina Mungu kama mwandishi mkuu, na kwa hivyo haina kasoro. Inadhihirisha upendo wa Mungu na kanuni ambazo anatumia kutuhukumu; na itabakia katika mwisho wa ulimwengu kama kiwango kikuu amabacho matendo ya binadamu, sheria na maoni ya kidini yanapaswa kujaribiwa. Inatosha kama njia yetu ya kipekee ya imani na matendo.

(1wakorintho 2:7-14; 2petero 1:20-21; 1wakorintho 2:13; 1wathesalonike 2:13; 2timotheo 3:16-17; mathayo 5:18, 24:35; yohana 10:35; waebrania 4:12; zaburi 119:89)

Maandiko:

- Yameongozwa kiungu (2timotheo 3:16) (Mungu alitoa pumzi)
- Yana uhakika (mithali 3:20-23) (ina uhakika, ina tumanini, inaaminika)
- Yenye asili (zaburi 19) haina dosari
- Ya kipekee (yuda 3)
- Imekamilika (yuda 3; waebrania 1:1 )

**Kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya imani katika Mungu na wakati katika maandiko.**
Tunavyojua mengi zaidi kuhusu Mungu, imani yetu katika Mungu inakua. Tunapoona yale ametenda, tunapoelewa yeye ni nani, tunapohukua muda kupata kujua moro wake- imani yetu inakua dhabiti.
Kama tulivyoarifiwa awali, Biblia ni ufunuo wa Mungu kuhusu yeye. Katika maandiko yafuatayo, utatambua uhusiano kati ya imani, wakati katika maandiko na maandiko yakimdhihirisha Mungu.

- Warumi 10:17 "chanzo cha imani ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la Kristo" Imani yetu inaongezeka kwa sababau neno la Mungu linamlenga mwana wa Mungu.
- Katika Yohana 5:39, Yesu aliwaambia watu wa kidini, "munatafuta maandiko kwa maana mnadhnai kuwa mtapata uzima wa milele"haya ndi yanayotoa ushuhuda wangu..." kwa maneneo mengine, maandiko yanamlenga Kristo. Neno la Mungu linamlenga mwana wa Mungu.
- Katika matendo 8:35 philipo alikuwa akiongea na towashi wa Uhabeshi kuhusu andiko katika Isaiah. Inasema, "basi Philipo akafungua kinywa chake na kutoka kwa maandiko akamhubir ia yesu... " Philipo angewezaje kuhubiri Yesu kutoka katika kitabu cha Isaiah? Isaiah iliandikwa zaidi ya miaka 600 kabla ya kuzaliwa kwa Yesu. Jibu ni kuwa, maandiki ya kinabii ya Isaiah yalimlenga Kristo. Neno la Mungu linamlenga mwana wa Mungu.
- Katika Yohana 1:1, inasema, "hapo mwanzo kulikuwa na neno naye neno alikuwa Mungu, naye neno alikuwa Mungu". Yohana 1:14 inasema, naye neno alifanyika mwili, na akakaa kwetu, nasi tukauona utukufu wake, utukufu kamawa mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na ukweli." Yesu ndiye wa pekee katika maandiko ambaye anatambulika kama "mwana wa pekee wa Baba". Neno la Mungu linamlenga mwana wa Mungu.

- Katika Wagalatia 3:24 , Paulo alisema, "basi torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa kristo, ilituhesabiwe haki kwa imani".torati (mwanzo-torati) ilikuwa ni mwalimu wetu. Paulo anatuambia kuwa sheria ya agano la kale lilituelekeza kwake Kristo. Neno la Mungu linamlenga Yesu Kristo.

Biblia ni ufunuo wa Mungu kuhusu yeye. Anatueleza kuhusu tabia zake. Anashiriki sehemu ya mipango yake. Unaposhiriki wakatika katika Biblia, utapata kujua akili, moyo na utu wa Mungu. Unapoendelea, imani yako itaongezeka.

**Kuna njia mingi za kusoma Biblia.** Kusoma Biblia kote sio sawa. Watu husoma Biblia kwa sababu ya:

- Burudani: wanasoma kwa kujifurahisha
- Utumizi: wanasoma ili kupata ufunuo katika maisha
- Mafunzo : wanasoma ili kushiriki pamoja na wengine
- Kujifunza: wanasoma ili kupata ujuzi
- Kujitoa kwa Mungu: wanasoma ili kumjua Mungu.

Kila njia ina manufaa; hata hivyo, wakati wako wa kipekeeni muhimu kwa ajili ya kujitoa kwa Mungu(kusoma Biblia ili kumjua Mungu).

**Kanuni muhimu za kusoma Biblia:**

Ili kuelewa na kutafsiri maandiko kwa njia ifaayo,tunapaswa kujua muktadha. Unatambua muktadha kwa kukujua ni nini ambacho mwandishi halisi alimnenea msomaji halisi na kwa sababu hiyo halisi. Usipojua ni nini kilichosemwa hapo awali, huwezi kujua ni nini cha kuweka katika matendo sasa hivi.

**Ninaelewaje muktadha wa maandiko?** Uliza maswali 5:

- Mwandishi: ni nani alikuwa mwandishi halisi?
- Msikilizaji: ni nani alikuwa msikilizaji halisi?
- Mazingira: mazingira halisi yalikuwa ni yapi?
- Kusudi: kitabu hiki kiliandikwa kwa nini? (mf. Wagalatia, mariko, ufunuo)
- Namna: ni nini mtindo wa uandishi? (mf shahiri, maandiko ya kihistoria, fasihi ya busara)

Baadhi ya ujumbe huu unapatikana katika mwanzo wa kitabu katika Biblia ya kusoma. Kwa ujumbe zaidi wa Biblia, usomi wa Biblia na kutafsiri maandiko, tazama kiambatisho cha 1, 2 na 3 mwisho wa nakala.

**How do I apply the Scriptures to my life?**

- Observation: What does the passage say?
- Interpretation: What does the passage mean?
- Application: How does the passage apply to me?

**Nitaanza aje?** Unapopata Biblia ambayo ni rahisi kusoma, haya ni mawazo kadhaa…

- UPiga mstari, na uandike chini pointi muhimu kando ya daftari.unaweza rekodi yale ambayo Mungu anafunza.
- Soma kwa kina, sio umbali
- Unapaswa kuanza wapi?
    - o Anza na mambo amabayo Mungu analeta akilini mwako (mf mf: fedha, imani, hasira)
    - o Soma Mithali; soma mlango amabo unalingana na siku hiyo ya mwezi
    - o Soma Injili na utazamie tabia na maisha ya Kristo
    - o Soma Nyaraka na udadisi jinsi injili huishiwa katika maisha ya kila siku.
    - o Soma Biblia katika mwaka (kwa kutumia Biblia ya mwaka mmoja)
    - o Chukua katika mtandao (YouVersion Bible App) itakupa mipango tofauti kadhaa za kusoma maandiko.

# SEHEMU YA 6: *Ninapaswa Kujua Nini Kuhusu Maombi?*

## *Wazo kuu:*

**Maombi ni mazungumzo na Mungu, tunanena na kusikiliza.**

**Mukhtasari:**

✦ **Injili ni habari njema ya Mungu ambayo unaokoa na kumsafisha mtu. Huwezi kukua kuzidi injili.**

✦ **Ukristo unahusu uhusiano.**
Kuna uhusinao tatu kuu: uhusiano na Mungu, Kanisa na Ulimwengu. Chochote ambacho Mungu ana shauku ya kutenda katika maisha yako, atatimiza kutokana na kuzidi kwa uhusiano wako pamoja naye.

✦ **lengo kuu ni kumjua Mungu kwa kushiriki muda pamoja na Mungu.**

✦ **Kushiriki wakati na Mungu kunapaswa kutiwa motisha na upendo.**

✦ **Maandiko ni amri ya mwisho kwa imani zote, na matendo.**

Maombi ni mazungumzo na Mungu. Haitatanishi. Haipaswi kuwa ya kupendeza au kishahiri. Haihitajiki kuwa ndefu au yakughadhabisha, maombi ni mazungumzo na Mungu.

Biblia , kwa uwazi inwafunza wakristo jinsi ya kuomba. Tuyagawe mazunguzo katika sehemu mbili. (1) Kuzungumza na Mungu (2) kumsikiliza Mungu

Wakristo wengi hutumia muda wao mwingi katika sehemu ya kwanza. Tunazungumza kwake Mungu. Tunashiriki shida zetu, maswali, furaha na mengine.

Kuna sehemu kadhaa muhimu za kuzungumza na Mungu.

1. **Maombi:** kuongea na Mungu kwa jumla
2. **Dua:** kumwomba Mungu hitaji la kibinafsi
3. **Kuombea:** kumwomba Mungu kuingilia kati kwa niaba ya mtu mwengine
4. **Sujudu:** kushiriki upendo na heshima kwake Mungu
5. **Shukrani:** kutoa shukrani kwa yale ambayo Mungu ametenda
6. **Sifa:** kuthamini yale Mungu ametenda

Ingawa kuna vijisehemu vingine vidogo, hizi ndio njia muhimu za kuongea naye Mungu. Katika sehemu hizi zote, tunatenda mazungumzo.

Maombi hayapaswi kuwa mazungumzo ya kipekee, yanapaswa kuwa mazungumzo ya ana kwa ana. Hatupaswi tu kushiriki moyo wetu na Mungu; tubapaswa kusikiliza, wakati Mungu anashiriki Moyo wake pamoja nasi.

Kumsikiliza Mungu katika maombi kunachukua muda. Inachukua muda kusikiliza sauti yake. Inachukua muda kutofautisha kati ya kile Mungu alisema na kile unachodhani kuwa alisema. Unavyosikiliza zaidi na unavyoshiriki muda wako zaidi, ndivyo sauti yake inakuwa dhahiri.

## Tunawezaje kukua katika uwezo wetu wa kusikia sauti ya Mungu?

1. **Tunavyoshiriki muda wetu zaidi pamoja na Mungu katika maombi, ndivyo tunaweza kutambua sauti ya Mungu.**

   Tafakari uhusiano ulio katibu nasi. Jinsi uhusiano unavyokua karibu, ndivyo sauti inakua ya kutambulika! Kuna watu amabo wanakupigia simu lakini hawahitaji kujitambulisha (mf; wazazi, wachumba, watoto, ndugu, marafiki wa karibu) kuna uzoefu unaotokea tu kwa kuzidi kukaa pamoja.

   Hiyo ni sawa na kwake Mungu. Zadi tunavyozungumza na Mungu na kusikiliza anachosema-ndivyo tnavyopata uzoefu wa sauti ya kinywa chake.

2. **Tazamia zaidi kwa mambo unayosikia kuliko jinsi sauti hiyo inavyotoka.**

   Kuna uwezekano wa mkanganyo kati ya kusikia sauti ya Mungu na kutambua ni nini ambacho Mungu anasema. Ya kwanza ni ngumu kuliko ya pili.

   Kwa mara nyingine, tazama mazungumzo ya binadamu. Sauti ya mamako ikoje? Mtu anaweza sema ni ya kike, ina pendeza. Anaongea kwa kiinitoni. Ana sauti nyororo. Hivyo ni vyema, lakini umefupisha uwezekano kwa watu wengine bilioni moja.

   Sasa, mamako anaweza kusema nini kuhusu uongo, utakatifu, neno la Mungu, familia, afya, n.k?zaidi unavyomjua mamako, ndivyo utajua zaidi anachofikiria. Ikiwa unajaribu kutambua sauti yake, utaanza kwa kutoa mambo amabyo hayahusiani naye.

   Hayo ni sawa kwa Mungu. Tunapotazamia tunayosikia, tunaweza kulinganisha na kile alicho. Wakti wazo linagongana na asili yake, au neno lake, tunaweza kuondoa hayo katika yale tuliyotaja.

   Ikiwa una wakati mgumu kutambua hisia za kusikiliza, chati hii itakusaidia. Chati hii ilitolewa kutoka "kuchagua mazuri ya Mungu"

| **Sauti ya Mungu**: | **sauti ya shetani**: |
|---|---|
| Inakuongoza | inakuharakisha |
| Inakuhakikishia | inakusukuma |
| Inakutia moyo | inakuogopesha |
| Inakutuliza | inakukanganya |
| Inakupa mwanga | inakushusha moyo |
| Inakuliwaza | inakutia wasiwasi |
| Inakudhibitisaha | inakuhukumu |

3. **Pata uhakika kwamba unachosikia kina amabtana na maandiko.**

   Biblia ni neno la Mungu lililodhihirika. Kituo chetu cha kwanza katik akujifunza kutambua sauti ya Mungu kinapaswa kuwa kutambua ni nini Mungu ameandika tayari. Mungu hawezi kujikanganya. Hawezi kukuambia jambo katika maombi ambalo haliambatani na neno lake.

4. **Tazama maombi pamoaj na njia zingine za Mungu za kuongea na watu wake.**

   - Maandiko
   - Mapito ya kawaida
   - Mafunzo ya kiungu

   Kama sheria ya jumla,unachosikia katika maombi kinapaswa kuthibitishwa na maandiko, mafunzo ya kiungu na maito ya kawaida. Mungu ananuia kutumia hayo yote pamoja kuhibiti msimamo wake.

**Maombi ni mazungumzo pamoja na Mungu; tunanena na kusikiliza.**

# SEHEMU YA 7: *Mfuasi ni nani?*

## *Wazo kuu:*

**Mfuasi ni zaidi ya muumini aliyeelimika;**
**Mfuasi hutaka kuwa kama Kristo.**

**Mukhtasari:**

✦ **Injili ni habari njema ya Mungu ambayo unaokoa na kumsafisha mtu. Huwezi kukua kuzidi injili.**

✦ **Ukristo unahusu uhusiano.**

Chochote ambacho Mungu ana shauku ya kutenda katika na kupitia maisha yako, atatimiza kutokana na kuzidi kwa uhusiano wako naye.

✦ **lengo kuu ni kumjua Mungu kwa kushiriki muda pamoja na Mungu**

✦ **Kushiriki wakati na Mungu kunapaswa kutiwa motisha na upendo.**

✦ **Maandiko ni amri ya mwisho kwa imani zote, na matendo.**

✦ **Maombi ni mazungumzo pamoja na Mungu; tunanena na kusikiliza.**

## Mfuasi ni nani?

Yesu aliamuru Kanisa kuwakuza wafuasi. (mathayo 28:19-29) ikiwa hatuwezi kubainisha mfuasi, hatuwezi jua ikiwa tumekuza mfuasi. Wafuasi hubainishwa kama mwanafunzi, msomi au mfuasi wa Yesu. Kwa kimo cha kawaida, hiyo ni kweli. Hata hivyo mfuasi ni zaidi ya hayo tu. Maandiko yanambainisha mfuasi vipi? Tutazama mfuasi kulingana na karne ya kwanza.

Masomo ya kiyahudi ya karne ya kwanza yalikuwa na viwango kadhaa. Watoto walianza masomo yao kwa miaka 5 au 6 katika **Beth Sefer** (inamaana "chumba cha kitabu") . mafunzo yalilenga Torah (vitabu 5 vya kwanza vya Biblia)

Ilisemekana kwamba siku ya kwanza ya darasa, rabbi alichukua asali na kufunika daftari ya kila mtoto. Baadaye angewaambia wailambe asali hiyo. Na watoto walipoiramba asali rabbi alinukuu Zaburi 119:103 *"nayo maneno ya Mungu yawe matamu kuliko asali"* rabbi aliwataka watoto wajue kwamba hakuna jambo njema kama kuonja, kupokea na kufanya nenep la Mungu kuwa seemu ya maisha yako.

Kwa miaka 4-5 ifuatayo watoto hawa wange kumbuka maandiko mengi. Wengine walikariri Torah nzima misho wa Beth Sefer.

Baada ya Beth Sefer wanafunzi walikaa nyumbani kusaidia kazi za familia. Wazazi walitaka kuhakikisha kwamba watoto wao wametayarishwa kwa maisha ya usoni. Walihisi kuwa sehemu mbili za elimu ni muhimu; kuwelewa maandiko na mafunzo ya muda. Wanafunzi bora waliendelea na masomo yao **Beth Talmud** (chumba cha mafunzo)

katika Beth Talmud, masomo yalikuwa yenye mhemko zaidi. Walijifunza kuhusu manabii na maandiko. Walijifunza utafsiri wa Torah. Walijifunza jinsi ya kutafsirina kutenda maandiko. Walijifunza njia za kiyahudi za maswali na majibu.

Kiwango cha pili cha mafunzo kilitazamia ukweli wa kina na kuwa na tafakari zaidi. Mafunzo ya kiingereza hutazamia kubadilisha ujumbe. Baada ya kufunza hesabu za kuongeza, tunauliza maswali kama "ni nini 2 ukiongeza 2?" tunataka watoto wajibu "4" masomo yetu yameundwa kwa njia ambayo mwalimu anauliza swali na wanafunzi wanajibu.

Katika wakati wa yesu, rabbi walifunza watoto kujibu na swali. Mtazamio haukuwa tu wa kubadili ujumbe, ulikuwa katika kuelewa ujumbe huo. Rabbi anaweza sema ni nini 2 ukiongeza 2? Badala ya kujibu 4, mwanafunzi anaweza sema, "ni nini 8 ukitoa 4, au ni nini 25% ya 16?" ikiwa mwanafunzi angeweza kutoa jibu kwa njia ya swali, mwalimu alijua kuwa mwanafunzi ameelewa ujumbe. Yesu alikuwa katika kiwango hiki wakati ambapo wazazi wake walimpoteza katika hekalu

akiwa na miaka 12. (luka 2:46) inasema , *"...walimpata hekaluni akiwa ameketi kati ya waalimu akiwasikiliza na kuuliza maswali. Na wote waliosikia walishangazwa na kuelewa kwake na majibu yake"* hawakushangazwa na maswali yake, walishangazwa na kuelewa kwake na majibu yake. Maswali yake yalionyesha jinsi alivyoelewa ukweli.

Wakati mtoto alipomaliza Beth Talmud, baadhi yao wangekariri maandiko yaote ya agano la kale.

Mwisho wa Beth Talmud, watoto wengi hawakuendelea na masomo yao. Hata hivyo, wengine waliendelea kwa kiwango kilichofuata kilichoitwa **Beth Midrash** (chumba cha usomi) walipoingia hapa, waliitwa "talmidi" ina maana **"wafuasi"**.

Katika kiwango hiki, mwanafunzi angeenda kwake rabbi na kusema, "Rabbi, ninataka kuwa mmoja wa talmidin wako, tafadhali niruhusu katika chumba cha usomi" rabbi angeuliza maswali ili kupima kiwango chao cha elimu na kuelewa kwao.

Maswali yaliyoulizwa hayakuwa "unaweza kuniambi vitabu vya Torah? Au nani alitupwa katika shimo la samba?" rabbi angesema, katika Habakkuk kuna marejeleo manne ya Kumbukumbu la torati. Nitajie yote mfululizo" njia nyingine ilikuwa ni "remez"bila ya maandiko mbele yao, mwanafunzi alipaswa kujua msitari huo, na mistari liyofuata, muktadh awa mistari hiyo, kusema ikiwa msitari huo ulinukuliwa vyema.

Rabbi alitaka kujua ikiwa mtoto alifahamu Torah. Lengo lake lilikuwa ni kuona ikiwa mtoto alielewa mafunzo yake na ikiwa angewafunza wengine.

<u>**Kuelewa maandiko kwa kila Rabbi kuliitwa nira yake.**</u> ikiwa Rabbi aliamini kuwa mtoto huyo angeweza kuelewa na kuwafunza wengine, angesema, "njoo, nifuate". Kukubalika na Rabbii likuwa ni jambo la utukufu. Wakati huo, kijana huyo angeiacha familia yake, kazi, kitongoji na marafiki zake.

Lengo lake lilikuwa rahisi. **Alitaka kuwa kama Rabbi wake.** Luka 9:40 inasema "wanafunzi sio wakuu kuliko waalimu wao, lakini mwanafunzi aliyefunzwa vyema atakuwa kama mwalimu wake" wafuasi walifuata kila kitu ambacho rabbi alitenda. Walikula chakula sawa, walilala sehemu sawa, Walitembea sawa, n akuwa na tabia sawa. Rabbi alipoifunza nira yake, wafuasi walitazama, kusikiza na kutenda chochote alichotenda.

Je, umeona sababu ambayo njia za kisasa za kukuza wafuasi zimefeli? Tunamsawazisha mfuasi na kuwa tu mwanafunzi. Mwanafunzi hutaka kujua ambacho mwalimu anajua ili atoe jibu sahihi. Lakini hiyo sio maana ya kutaka kuwa mfuasi.

Mfuasi hutaka kuwa kama rabbi. Huo ni mpango wa Mungu kwa kila mkristo., anataka tuwe kama Kristo. Warumi 8:29 inasema "maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili ili wafanane na mwana wake" wagalatia 4:19 paulo alifanya kazi na wagalatia "mpaka Kristo awe nadani yako"

Wakristo hawafuati njia sawia ya ufuasi (Beth Sefer, Beth Talmud, Beth Midrash) tunaweza kuona somo la jumla. **Ufuasi hauhusu tu ujumbe; unahusu kubadilishwa. Lengo la Mungu sio kutufanya kuwa wasomi kibiblia, lengo lake ni kutufanya kama yeye.**

Je, ni nini maana ya kibibli ya ufuasi? <u>Mfuasi ni mfuataji anayeshiriki wakati wake pamoja na rabbi wake (akisikiliza, kutazama, na kutenda kama yeye) ili wawe kama yeye, na baadaye kupitisha mafunzo haya kwa wafuasi zaidi</u>.

**Mfuasi ni zaidi ya muumini aliyeelimika;**
**Mfuasi hutaka kuwa kama Kristo.**

# SEHEMU YA 8: *Ina maana gani kumfuata Kristo?*

## *Wazo kuu:*
### Kumfuata Kristo ni kuwa kama Kristo.

**Mukhtasari:**

- **Injili ni habari njema ya Mungu ambayo unaokoa na kumsafisha mtu. Huwezi kukua kuzidi injili.**
- **Ukristo unahusu uhusiano**
- **lengo kuu ni kumjua Mungu kwa kushiriki muda pamoja na Mungu**
- **Kushiriki wakati na Mungu kunapaswa kutiwa motisha na upendo.**
- **Maandiko ni amri ya mwisho kwa imani zote, na matendo.**
- **Maombi ni mazungumzo pamoja na Mungu; tunanena na kusikiliza.**
- **Mfuasi ni zaidi ya muumini aliyeelimika; mfuasi hutaka kuwa kama Kristo.**

## Mungu anataka nini kutoka kwangu?


Yesu alitumia maneno mawili kujibu hili swali. Nifuate mimi! Ni zaidi ya kusema wewe ni mkristo, kuenda kanisani na kujifunz hadithi za Biblia. Ni zaidi ya kupendezwa na maisha yake namafunzo yake.

<u>Kumfuata ni kuwa kama yeye</u>. Inhudu kushiriki wakati pamoja naye (kumsikiza, kumtazama na kutend akama yeye) ili tuweze kuwa kama yey, na kupitisha mafunzo kwa wafuasi zaidi.

kumfuata Kristo ni rahisi kuliko kumfuata rabbi mwingine. Wafuasi wa karne ya kwanza walitaka kuwa kama Rabbi wao kwa sababu Rabbi hao walitaaka tu kumfurahisha Mungu. Rabbi hawa walifuata torati lakini bado walikuwa wenye dhambi. waliunda nira zilizo kanganya na sheri za ziada ili kuhakikisha kuwa walitii Torah. Matokeo yalikuwa ni nira uliokuwa na uzito. Uhusiano huo ulifanana hivi:

**Mungu**
|
Sheria
|
Nira ya Rabbi
|
**Rabbi**
|
Nifuate
|
**Mfuasi**
|
Mwaka wa masomo

Namna hiyo ilikuwa ya kukanganya. Kumfuata Mungu, kumfurahisha Mungu, na kumtii Mungu- mfuasi alianza kwenye kina cha namna hii. Baada ya miaka ya masomo, wangekuwa wafuasi. Ili wawe kama rabbi, walihitajika kumfuata rabbi, kufuata nira yake, kufuata sheria na ilitosha kumfurahisha Mungu.




Kumfuata Yesu hakukanganyi. Yesuni Mungu. Yesu alitii sheria. Nira yake ni rahisi na mzigo wake ni mwepesi. (mathyo 11:28-30) hatutii sheria ili kupata haki na Mungu. Tumepata haki na Mungukupitia rabbi wetu. Kwa mfuasi wa Kristo mtiririko ni wa mviringo.

Yesu anatuambia tumfuate. Tunapofuata, (au kuishi ndani yake,) tunakuwa kama yeye (1yohana 15:1-10). Ni rahisi hivyo.

Kumfuata Kristo ni kuwa kama Kristo. Je, maisha yako yanakuwa kama yake? je ,moyo wake unaonekana maishani mwako? Je, unawapenda wengine? Je, unautazamia ufalme wake? Je, unatumikia alivyotumikia? Je, unafuata mfano wake wa kushiriki wakati pamoja naye Baba?

**Nakala ya ziada:**

# SEHEMU YA 9: *Wafuasi hukuzwa vipi?*

## *Wazo kuu:*

**Wafuasi hukuzwa wakari amabapo watu wanafuata Kristo kwa kumpenda Mungu, kuungana na waumini, kuutumikia ulimwengu na kuithamini injili.**

**Mukhtasari:**

- ✦ **Injili ni habari njema ya Mungu ambayo unaokoa na kumsafisha mtu. Huwezi kukua kuzidi injili.**
- ✦ **Ukristo unahusu uhusiano**
- ✦ **lengo kuu ni kumjua Mungu kwa kushiriki muda pamoja na Mungu**
- ✦ **Kushiriki wakati na Mungu kunapaswa kutiwa motisha na upendo.**
- ✦ **Maandiko ni amri ya mwisho kwa imani zote, na matendo.**
- ✦ **Maombi ni mazungumzo pamoja na Mungu; tunanena na kusikiliza.**
- ✦ **Mfuasi ni zaidi ya muumini aliyeelimika; mfuasi anataka kuwa kama Kristo.**
- ✦ **Kumfuata Kristo ni kuwa kama Kristo.**

## Je, wafusi hukuwa vipi? Ina maaana gani kumfuata Kristo?

Ikiwa ungemuuliza mkristo wa makamo jinsi ambavyo wafuasi hukuzwa, mazungumzo hayo yanaweza yakageuka kuwa mkusanyiko wa kikundi. "tunayo idara nzuri ya shule ya jumapili" au "tuna makundi madogo ambayo hukutana wiki nzima" hata ingawa wafuasi hukuzwa katika jamii, huo sio tu upeo wa kukuza wafuasi.

Hili ni swali kuu kwa kila mkristo. "Yesu aliwakuzaje wale 12?" je alikutana nao kwa masomo ya Biblia mara moja kila wiki? Alifanya nini?

Miaka kadhaa iliyopita, wafanyikazi wetu walifanya namna ya Yesu ya kukuza wafuasi kuwa kama tazamio la kipekee wakati wa kufunga. Tuliandika chini kila kitu ambacho tuliona Yesu akifunza au kufanya na wale 12. Pia tuliandika jinsi Paulo aliwakuza wafuasi Timetheo. Tito, Yohana, na wengine. Baadaye tuliyaweka katika makundi chini ya vichwa 4 vikuu. Baada ya kumaliza, tuliandika haya:

**Wafuasi hukuzwa wakat ambapo watu wanmfuata Kristo kwa kumpenda Mungu, kuungana na waumini, kutumikia ulimwengu na kuikabidhi injili.**

**Penda, ungana, tumikia, kabidhi.** Tuliongeza mambo haya pia.

**Katika kumpenda Mungu, tuliongeza…**

- Kufurahia uhusiano wa ndani na Mungu
- Kupata kumjua Mungu kupitia neno lake
- Kuongea na Mungu kupitia maombi
- Kushiriki muda pamoja naye Mungu
- Kumwabudu

**Katika kuungana na waumini, tuliongeza…**

- <u>Jamii ya kikristo</u>. Katika Agano Jipya, waumini walifurahia maisha pamoja. Yesu na Paulo walisafiri pamoja na wafuasi wao, walikula pamoja, wakatumikia pamoja, wakasoma maandiko pamoja. Walishiriki muda wao pamoja.
- <u>Maish a yaliyoungana</u>. Wafuasi wa Agano Jipya waliungana katika misheni, maombi, huuma, maono, upendo, kusoma Biblia. Wakukusanyika tu katika kundi, waliungana kati malengo sawia.
- <u>Upendo wa kweli</u>. Upendo kwa waumini wengine uliwabainisha watu kama wafuasi wa Yesu.

**katika kuutumikia ulimwengu tuliongeza…**

- Kuwaonyesha watu upendo kupitia matendo yetu-sio tu maneno yetu
- Kufuata mfano wa Kristo wa kuwatumikia wengine
- Kuwekeza ndani ya watu, familia, jamii na mataifa

**Katika kuikabidhi injili tuliongeza…**

- Kushiriki Injili pamoja na ufalme
- Kuyakabidhi mafunzo ya Kristo kwa wengine
- Kuwaalika wengine kujiunga na mambo ya Ufalme wa Mungu
- Wafuasi kuwakuza wafuasi

Wanafunzi hupenda, huungana, hutumikia na kukabidhi. Mambo mengine pia yalijitokeza.

1. Tuligundua kuwa uhusiano 3 kuu za wakristo zinaonekana: uhusiano wetu na Mungu ni wa kwanza, uhusiano wetu na kanisa ni wa pili na uhusiano wetu na ulimwengu uko katika pointi mbili za mwisho.
2. Matamshi yanaelekezwa kwa matendo. Matamshi yote yana neno a kutenda. UPENDO, UNGANA, TUMIKIA, KABIDHI. Haya yote ni maneno ya kutenda.
3. Kuwakuza wafuasi kunahitaji kushiriki wakati pamoja. Yesu alifunza maisha ya upendo, kuungana, kutumikia, kukabidhi- aliishi maisha hayo pamoja nao. Mtindo huo unaonekana wakati Pauloo aliwekeza ndani ya Timotheo, Luka, na Tito. Paulo alishiriki wakati pamoja na wale aliofanya wafuasi.

Unaweza kuongoza umati kwa umbali. Unaweza kuwafunza waumi ni kwa umbali. Lakini huwezi kuwakuza wafuasi kwa umbali. Kuwakuza wafuasi kunahitaji wakati pamoja.

Safari ya kila mtu na Mungu itakuwa tofauti, lakini njia ya wafuasi katika maisha ni sawia. Wafuasi wanamfuata Kristo kwa kumpenda Mungu, kuungana na waumini, kutumikia ulimwengu na kuikabidhi injili




Maelezo haya yanaweza kuwa kama dira ya kiroho. Ukitaka kuhakikisha kuwa mwenendo wa maisha yako unaelekea kwa ukuaji kama mfuasi, weka ukweli huu juu ya maisha yako na umuulize Mungu akuongoze. Mungu lazima abakie kuwa “kaskazini yetu ya kiroho” chochote kingine kunatokana n auhusiano wetu. Ukijipata katika uwanda wa juu wa kiroho, uliza, “je ni nini kinakosa?” ukijipata unapiti mnyauko wa kiroho, weka dira hii ya kiroho juu ya maisha yako. Utagundua kuwa mojawapo ya sehemu hizi zinakosa au haizitumiwi ipasavyo.

Dira ya kiroho inaweza kutoa maono katika safari yako na Mungu. Inaweza kukusaidia kuona hatua zinazohitajika kenda katika kiwango kifuatacho..inaweza pia kukusaidia kutambua ulipo na hatua uanazohitaji katika ukuaji wa baadaye.

**Wafuasi hukuzwa wakari amabapo watu wanafuata Kristo kwa kumpenda Mungu, kuungana na waumini, kuutumikia ulimwengu na kuithamini injili.**

# SEHEMU YA 10: *Wewe ni nani?*

## *Wazo kuu:*
## kitambulizi chako kipya kinapatikana katika Kristo.

**Muhtasari:**

- **Injili ni habari njema ya Mungu ambayo unaokoa na kumsafisha mtu. Huwezi kukua kuzidi injili.**
- **Ukristo unahusu uhusiano**
- **lengo kuu ni kumjua Mungu kwa kushiriki muda pamoja na Mungu**
- **Kushiriki wakati na Mungu kunapaswa kutiwa motisha na upendo.**
- **Maandiko ni amri ya mwisho kwa imani zote, na matendo.**
- **Maombi ni mazungumzo pamoja na Mungu; tunanena na kusikiliza.**
- **Mfuasi ni zaidi ya muumini aliyeelimika; mfuasi anataka kuwa kama Kristo.**
- **Kumfuata Kristo ni kuwa kama Kristo**
- **Wafuasi hukuzwa wakari amabapo watu wanafuata Kristo kwa kumpenda Mungu, kuungana na waumini, kuutumikia ulimwengu na kuithamini injili.**

## Ina maana gani kuwa kitambulisho chako kinapatikana katika Kristo?

Kitambulisho chetu ndicho kinatubainisha. Kitambulisho chetu kina husiana na mambo tunayofanya, tunachopenda, tulipo au jinsi tunavyojiona. Tafakari jinsi watu hujitambua katika kundi.mtu anaweza sema"mimi ni Yohana, nina miaka 34 na nina uraibu wa ulevi" kitambulisho chake kinahusiana n ajinsi anavyojiona. Mwingine anaweza sema "jina langu ni Allie, nilihitimu katika shule ya MIT na shahada ya uasisi" kitabulisho chake kinahusiana na mambo ambayo amefanya.

Kabla ya Kristo, kitambulisho chetu cha kiroho kilibainishwa kwa neno moja-dhambi. Ikiwa tungejitambulisha katika kundi la kiroho, tungesema, "jina langu ni________ mimi ni mwenye dhambi" dhambi ulitubainisha. Dhambi ilibainisha hali yetu iliyopita; dhambi ilibainisha makabiliano yetu; dhambi ilibainisha ukweli wa maisha ya usoni.

Watu wengi hawangesema "sijawahi kutenda dhambi" hata hivyo, watu wengi wako tayari kusema kiwango cha matendo yao. "kweli nilitenda dhambi, lakini haikuwa mbaya sana. kuna wengi ambao wametenda maovu zaidi yangu". Ingawaje kuna matokeo tofauti kwa kila dhambi (mbele ya mahakama), dhambi ni dhambi mbele ya Mungu.

Tafakari haya. Mtu akichukua pakiti ya gamu na akose kuilipia, jamii inamwita mwizi. Wakati wa kosa hilo, wanatambulika kwa kuiba. Haijalishi ikiwa waliiba pakiti ya gamu au gari au pesa. Mtu akichukua kitu ambacho sio chake, ataitwa mwizi. Hiyo ni sawa pia katika dhambi. Haijalishi ikiwa mtu ametenda dhambi kwa njia ndogo, au kubwa.

Warumi 3:23 "wote wametenf=da dhambi, na kukosa utukufu wake Mungu" katika hali yrtu ya kuanguka, kila mtu anitwa mwenye dhambi, machoni pa Mungu. Hata hivyo, msalabani, Yesu alilipia gharama ya dhambi, alisamehe deni yetu ya dhambi. Katika 2wakorintho 5:17 "mtu akiwa ndani ya Kristo, yeye ni kiumbe kipya, mambo ya kale yamepita, mambo mapya yakaja." Yesu hakusafisha kitambulisho chetu cha zamani, ametupa kitambulisho kipya ***katika Kristo***.

Kabla ya Kristo tulitambulika kiroho kama wenye dhambi. Katika Kristo tunatambulika kama watakatifu. Yesu alitupa kitambulisho kipya ndani yake. hautambuliki tena kwa mambo ambayo umetenda (mema au mabaya) unbainishwa na Yule Kristo aliye. Wewe ni kile asemacho ulicho. Kitambulisho chako (maisha yako) kinapatikana katika Kristo (wakolosai 3:3-4)

Sehemu muhimu ya maisha ya ukristo ni kujifunza kujiona jinsi Mungu atuonavyo. Sio rahisi. Watu hujaribu kutubainisha. Maisha yetu ya kale hujaribu kutubainisha. Sisi hutaka kujibainisha. "mimi ni mchungaji, mwalimu, mwana biashara, rubani, meneja wa benki" hii haifai kulingana na kiroho. Kazi ni kile unachofanya, sio ulicho. Maisha ya kale ni kile tulichokua; sio kile tulicho sasa. Ukiwa ndani ya Kristo, wewe ni kiumbe kipya. Kitambulisho chako kinapatikana katika Kristo.

Lazima tukubali kitambulisho chetu kibainishwe na Mungu. Orodha hii inaonyesha wewe ni nani kulingana na Mungu.

## Wewe ni nani?

**Nyinyi ni chumvi ya dunia na nuru ya ulimwengu** (mat 5:13, 14)

**Wewe ni mwana wa Mungu** (sehemu ya familia yake Yohana 1:12; Waumi 8:16)

**Wewe ni sehemu ya mzabibu wa kweli** (Yohana 15:15)

**Wewe ni rafiki ya Kristo** (yohana 15:15)

**Umechaguliwa na Kristo kubeba matunda yake** (yohana 15:16)

**Wewe ni shaidi wa Kristo** (matendo 1:8)

**Wewe ni mtumwa wa haki** (warumi 6:18)

**Wewe ni mwana wa Mungu** (warumi 8:14, wagalatia 3:26; 4:6)

**Wewe ni mrithi pamoja na Kristo** (warumi 8:17)

**Wewe ni hekalu ya Mungu** (1wakorintho 3:16; 6:19)

**Umeunganishwa naye Bwana** (1wakorintho 6:17)

**Wewe ni sehemu ya mwili wa Kristo** (1wakorintho 12:27; waefeso 5:30)

**Wewe ni kiumbe kipya** (2wakorintho 5:17)

**Umepatanishwa kwake Mungu** (2wakorintho 5:18; 19)

**Wewe ni mwana wa Mungu na na moja katika Kristo** (wagalatia 3:26, 28)

**Wewe ni mtakatifu** (waefeso 1:1 1wakorintho 1:2, wafilipi 1:1 wakolosai 1:2)

**Wewe ni kazi ya Mungu** (waefeso 2:10)

**Wewe ni mwananchi pamoja na watu wa Mungu** (waefeso 2:19)

**Wewe ni mfungwa wa Kristo** (waefeso 3:1, 4:1)

**Wewe ni mwenye haki na mtakatifu** (waefeso 4:24)

**Wewe ni mwananchi wa mbingu na umeketi mbinguni sasa** (wafilipi 3:20; waefeso 2:6)

**Umefichwa na Kristo katika Mungu** (wakolosai 3:3)

**Wewe ni kielelezo cha maisha ya Kristo** (wakolosai 3:4)

**Umechaguliwa na Mungu, mtakatifu na mpendwa** (wakolosai 3:12, 1wathesalonike 1:4)

**Wewe ni mwana wa nuru na sio giza** (1wathesalonike 5:5)

**Wewe ni ndugu mtakatifu** (waebrania 3:1)

**Wewe ni mshirika wa Kristo** (waebrania 3:14)

**Wewe ni mojawapo ya mawe yaliyohai ya Mungu** (1petero 5:8)

**Wewe ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu** (1petero 2:9,10)

**Wewe ni msafiri na mpitaji katika ulimwengu huu** (wewe ni adui ya shetani)

**Sasa wewe ni mwana wa Mungu** (1yohana 3:1, 2)

**Wewe ni mzaliwa wa Mungu na mwovu** (shetani) **hawezi kukuguza**

**Wewe ni kondoo wa malisho yake. una chochote unachohitaji** (zaburi 23 na 100)

Kitambulisho chetu kinapatikana katika Kristo. Soma matamshi haya pamoja na maandiko. Anza namna ya kuweka upya fikra zako kutumia ukweli huu. (wakolosai 3:10) orodha hii sio jambo la kusoma, kuamini na kupita. **Hili ni jambo ambalo utasoma, urudie kusoma na utafakari, uombe, na umwombe Mungu akukumbushe kuhusu – katika safari yako ya ukristo.**

**Kitambulisho chako kinapatikana katika Kristo.**

# SEHEMU YA 11: *Tunatembea vipi kama wafuasi?*

## *Wazo kuu:*

**Jinsi ulivyompokea Kristo ndivyo utakavyotembea ndani ya Kristo.**

**Muhtasari:**

- ✦ **Injili ni habari njema ya Mungu ambayo unaokoa na kumsafisha mtu. Huwezi kukua kuzidi injili.**
- ✦ **Ukristo unahusu uhusiano**
- ✦ **lengo kuu ni kumjua Mungu kwa kushiriki muda pamoja na Mungu**
- ✦ **Kushiriki wakati na Mungu kunapaswa kutiwa motisha na upendo.**
- ✦ **Maandiko ni amri ya mwisho kwa imani zote, na matendo.**
- ✦ **Maombi ni mazungumzo pamoja na Mungu; tunanena na kusikiliza.**
- ✦ **Mfuasi ni zaidi ya muumini aliyeelimika; mfuasi anataka kuwa kama Kristo.**
- ✦ **Kumfuata Kristo ni kuwa kama Kristo**
- ✦ **Wafuasi hukuzwa wakari amabapo watu wanafuata Kristo kwa kumpenda Mungu, kuungana na waumini, kuutumikia ulimwengu na kuithamini injili.**
- ✦ **kitambulizi chako kipya kinapatikana katika Kristo**

*"Therefore, as you have received Christ Jesus the Lord*, ***so walk in Him***." (Colossians 2:6)

## Je, unatembeaje katika Kristo (au kuishi ndani ya Kristo)?

Tunahitaji kurudi nyuma, na kuuliza swali: ulimpokeaje Kristo? Jibu linapatikana katika matamshi haya: kwa neema, umeokolewa kwa imani (waefeso 2:8) haukumpokea Kristo kupitia kazi njema. Hukumpokea Kristo kwa sababu ulimtambua au kufikiria kuwa katika familia ya Mungu. Hukumpokea Kristo kwa sababu ulizaliwa katika familia ya haki, au ulienda kanisa inayostahili.

Ulimpokea kristo kwa neema ya Mungu kwa sababu uliamini aliyosema kuhusu dhambi zako, utengano na Mungu, na hitaji lako la mwokozi. Ulimpokea Kristo kwa sababu uliamini kuwa Yesu alikufa msalabani kwa dhambi zako. Alifufuka tena kwa siku ya tatu, na anatoa uzima wa milele (uhusiano wa upatanisho) kwa watakao tubu kwa kuweka imani katika Kristo. Uliingia katika uhusiano kwa neema kupitia imani. **Neeme ni kile ambacho Mungu alitoa:imani ni jinsi ulivyoitikia.**

Lengo la maandiko ni "mwamini Bwana Yesu na utaokolewa" (matendo 16:31). Mungu anatoa neema; tunapaswa kuitika kwa imani. Ndio maana Waefeso inasema "kwa neema umeokolewa kupiti a imani". Yohana alisema "wngi waliompokea, aliwapa uwezo kuwa wana wa Mungu, na kwa walio amini jina lake" tulimpokea Kristo kwa neema kupitia imani. **Jinsi ulivyompokea Kristo ndivyo unavyotembea katika Kristo.**

Kutembea katika Kristo kuna sehemu mbili: neema na imani. Kielelezo cha neema ni kibali cha Mungu. Ingawaje, kielelezo hichi sio kamilifu. **neema ni matendo ya Mungu kwetu na ndani yetu, yale ambayo hatungeweza kutenda sisi wenyewe.**

- Hatungeweza kujiokoa. Lakini Mungu alitenda ndani yetu mambo ambayo hatungeweza
- Hatuwezi kuishi maisha ya kikristo, lakini Mungu anatenda ndani yetu mambo ambayo hatungeweza
- Hatuwezi kufanya kazi ya huduma, lakini Mungu anatenda yale hatungeweza kwa nguvu zetu (hiyo ni neema).

Tunatembea ndani ya Kristo kwa kujifunza kutegemea neema na sio nguvu zetu. Sehemu ya pili ya kutembea ndani ya Kristo ni imani.

Waebrania inatuambia kuwa "wenye *haki wataishi kwa* *imani... na bila* *imani ni vigumu kumfurahisha Mungu"* 2wakorintho 5:7 *"tunaishi kwa imani na sio kwa kuona"* wafuasi walipomuuliza Yesu jinsi wangeweza kuungana naye Baba katika mambo ya Ufalme, Yesu alisema "*hii ni kazi ya Mungu, kwamba muweze kumwamini Yule aliyemtuma*"

Tunapaswa kutembea kwa imani; tunapaswa kuishi kwa imani; tunapaswa kutenda kupitia imani. Ulivyompokea Kristo ndivyo utatembea katika Kristo.

Tuangalie mfano. Unakabiliana kudhibiti hasira yako, unamwomba Mungu aiponye ndoa yako, umelemewa na wokovu wa mwanao, unahitaji muujiza wa kufedha, unapambana na woga, upweke, majaribu, mawazo- utafanya nini?

Paulo anasema, "*ulivyompokea Kristo, tembea ndani yake*" ulimpokea vipi? Kwa neema umeokolewa kupitia imani! Unapaswaje kutembea ndani yake? kwa neema kupitia imani! Tegemea neema ya Mungu na utembee katik aimani.

Pointi ifuatayo ina uzito. **Biblia haipendekezi imani au matndo; hili ni jambo la kutenda kwa imani.** Yakobo 2:18 inasema "*mna imani nami nina matendo; nionyesheni imani yenyu bila matendo na nitawaonyesha imani yangu kwa matendo yangu*" imani dhabiti itadhiirika kwa matendo.

Kutembea kwa imani haimaanishi tunakataa kutenda. Ina maana tunatenda kwa kumjibu Mungu. Tunamwamini Mungu kuongoza; na anapoongoza, tunafuata. Tunamwamini Mungu kutoa, na anapotoa, tunapokea. Tunamwamini Mungu kutulinda; na anapotushawishi kuomba, tunashiriki muda wetu katika maandiko au kutafuta mawaidha ya kiungu- tunaitikia kwa utiifu. Matendo yetu yanatokana na imani.

## Jinsi ulivyompokea Kristo ndivyo utakavyotembea ndani ya Kristo.

**Nakala ya ziada:**

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

# SEHEMU YA 12: *Ni kwa nini kanisa ni muhimu?*

## *Wazo kuu:*

### Sehemu ya ukuaji wako katika Kristo inatendeka tu katika jamii.

**Muhtasari:**

- ✦ **Injili ni habari njema ya Mungu ambayo unaokoa na kumsafisha mtu. Huwezi kukua kuzidi injili.**
- ✦ **Ukristo unahusu uhusiano**
- ✦ **lengo kuu ni kumjua Mungu kwa kushiriki muda pamoja na Mungu**
- ✦ **Kushiriki wakati na Mungu kunapaswa kutiwa motisha na upendo.**
- ✦ **Maandiko ni amri ya mwisho kwa imani zote, na matendo.**
- ✦ **Maombi ni mazungumzo pamoja na Mungu; tunanena na kusikiliza.**
- ✦ **Mfuasi ni zaidi ya muumini aliyeelimika; mfuasi anataka kuwa kama Kristo.**
- ✦ **Kumfuata Kristo ni kuwa kama Kristo**
- ✦ **Wafuasi hukuzwa wakari amababpo watu wanafuata Kristo kwa kumpenda Mungu, kuungana na waumini, kuutumikia ulimwengu na kuithamini injili.**
- ✦ **kitambulizi chako kipya kinapatikana katika Kristo**
- ✦ **Jinsi ulivyompokea Kristo ndivyo utakavyotembea ndani ya Kristo**

## Ni nini umuhimu wa Kanisa?

**Je, kwa nini ni muhimu kuungana pamoja na waumini wengine?**
Jibu: sehemu yako ya ukuaji katika Kristo inatendeka tu katika jamii.

Ukristo ni spoti ya timu. Ukutaka kuwa jambo ambalo Mungu alikuumba uwe, inatendeka tu katika jamii ya kibiblia

Jamii ya kibiblia ni zaidi ya kuonekana kanisani siku ya jumapili. Ni zaidi ya kuhudhururia masomo ya Biiblia, au kula pamoja na mkristo mwingine. Inahusu kuunga maisha yetu katika lengo moja,na kuishi pamoja ka wananchi wa ufalme wa Kristo.

Wanafunzi 12 walipoitwa kumfuata Kristo, hawakuitwa kibinafsi kwa mafunzo ya mwaka mmoja. Waliitwa mpamoja kwa safari ya maisha.

- **Walikuwa pamoja katika ufuataji:**
  - o Yesu alipofunza, wafuasi walikuwa pamoja naye (mathayo 5:1-7:29)
  - o Yesu alipohudumu, wafuasi walikuwa pamoja naye
  - o Yesu alipoenda miujiza, wafuasi walikuwa pamoja naye (mathayo 8:23-27)

- **Walikuwa pamoja katika utumishi:**
  - o Yesu alipowalisha watu 5000 na 4000, wafuasi waliwapa chakula pamoja
  - o Yesu alipowatuma nje 12 na baadaye kuwatuma 70, aliwatuma wawili kwa wawili (mariko 6:7-13; luka 10:1-16) walitumikia pamoja.

- **Walikuwa pamoja na maswali:**
    - Hawakuelewa mafunzo magumu ya Kristo (mariko 8)
    - Walikuwa na maswali kuhusu kitambulisho cha Kristo (mathayo 8:27)
    - Hawakuelewa miujiza yake.

- **Walikuwa pamoja katika kujifunza:**
    - Bwana, tufunze jinsi ya kusali (luka 11:1-3)
    - Mahubiri milimani (mathayo 5-7)
    - Mafundisho ya mafumbo (mathayo 13)

- **Walikuwa pamoja katika upendo:**
    - 1 yohana 13:35-36, Yesu alisema, "*ninawapa amri mpya, kwamba mpendane, kama nilivyowapenda. Kwa hiyo, watu watajua kwamba ninyi ni wafuasi wangu*"

- **Walikuwa pamoja katika kutiana moyo:**
    - Katika luka 22:31, Yesu alimwambia Simoni, "*shetani amewataka nyinyi awapepete kama ngano; lakini nimekuombea wewe ili imani yako isitingike, nawe utakapoongoka, uwaimarishe ndugu zako*"

- **Walikuwa pamoja katika misheni:**
    - Yesu aliwaambia wafuasi katika Mathayo 28:19-20 "*nendeni mkafanye wafuasi katika mataifa yote, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, mkiwafunza kutii niliyowaamuru...*"

Wafuasi walikuwa pamoja katika kumfuata Kristo, wakiwa pamoja kwa ajili ya Yesu, katika maswali kuhusu Kristo, kujifunza kutoka kwa Kristo, katika upendo, katika kutiana moyo, katika misheni. Walisafiri pamoja, kula pamoja, na kuhudumu pamoja.maisha yao yalikuwa pamoja.

Mazingira yaliyowekwa na Krisst hayakuwa ya mashindano. Aliweka mazingira ambapo jami ilisaidia katika ukuaji. Hawakuwa peke yao. Waliwekwa katika jamii iliyowatia moyo, nguvu, urafiki na vipaji vingine.

**Sehemu ya ukuaji wako katika Kristo inatendeka tu katika jamii.**

**Additional Notes:**

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

# SEHEMU YA 13: *Ufalme wa Mungu ni nini?*

## *Wazo kuu:*

**Ufalme wa Mungu ni mambo yenye enzi ya Mungu ambao unaleta watu katika uhusiano ulio sawa na Mungu.**

Mukhtasari:

- ✦ Injili ni habari njema ya Mungu ambayo unaokoa na kumsafisha mtu. Huwezi kukua kuzidi injili.
- ✦ Ukristo unahusu uhusiano
- ✦ lengo kuu ni kumjua Mungu kwa kushiriki muda pamoja na Mungu
- ✦ Kushiriki wakati na Mungu kunapaswa kutiwa motisha na upendo.
- ✦ Maandiko ni amri ya mwisho kwa imani zote, na matendo.
- ✦ Maombi ni mazungumzo pamoja na Mungu; tunanena na kusikiliza.
- ✦ Mfuasi ni zaidi ya muumini aliyeelimika; mfuasi anataka kuwa kama Kristo.
- ✦ Kumfuata Kristo ni kuwa kama Kristo
- ✦ Wafuasi hukuzwa wakari amababpo watu wanafuata Kristo kwa kumpenda Mungu, kuungana na waumini, kuutumikia ulimwengu na kuithamini injili.
- ✦ kitambulizi chako kipya kinapatikana katika Kristo
- ✦ Jinsi ulivyompokea Kristo ndivyo utakavyotembea ndani ya Kristo
- ✦ Sehemu ya ukuaji wako katika Kristo inatendeka tu katika jamii

### What is the kingdom of God?

<u>Ufalme wa Mungu ni mambo yenye enzi ya Mungu ambao unaleta watu katika uhusiano ulio sawa na Mungu</u>. Hatutawahi kuelewa mpango mkuu wa Mungu katika ulimwengu ila tu tutakapo weka fikira zetu katika ufalme wa mbingu.

Tunaona kwamba ufalme wa Mungu ulikuwa katikati ya mafunzo ya Kristo. Yesu alikuja kutangaza injili ya Ufalme wa mbingu.

Mathayo 4:17 inarekodi ujumbe wa kwanz ambao Yesu alihubiri. "*tubuni, maana **ufalme wa Mungu** unakuja*" mathayo 4:23 inasema "*Yesu alienda Galileo nzima akifunza katika sinagogi n akutangaza injili ya **ufalme**...*"

Ukienda mathayo 5, utapata Mahubiri milimani. Ujumbe huu ungekuwa ujumbe mashuhuri kuwahi kuhubiriwa. Maneneo ya kwanza katika aya ya 3 yalikuwa, "*heri walio masikini katika roho, maana **ufalme wa Mungu** ni wao" aya ya 10"heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki, maana **ufalme wa Mungu ni wao***"

Aya ya 19 inahusu ufalme. Aya ya 20 inahusu ufalme. Sala iliyo katika mathayo 6 inaongea kuhusu ufalme. Jibu la Kristo kwa mahitaji yetu ni kutazamia ufalme na mambo yote yale yatatufuata (mathayo 6) kwa hakika, ufalme wa Mungu umetajwa mara nyingi sana kiasi kufanya mahubiri hayo kuitwa "katiba ya ufalme"

Yesu alihubiri ufalme wa Mungu katika sinagogi (mathayo 4:23) milimani (mathayo 5:7) kupitia mafumbo (mathayo 13) n akupitia maombi (mathayo 19:14) aliwatuma wafuasi na ujumbe wa ufalme (mathayo 6:9-13) aliwatumia watoto kuelezea wannchi wa ufalme (mathayo 19:14) na alitoa changamoto kwa kiburi kwa kuonyesha maana ya ukuu kulingana na viwangi vya ufalme (mathayo 18:1-5) alihutubu kuhusu huzuni kwa kuelekeza umakini wa wafuasi katika upatanisho wa ufalme ujao.

Yesu alikaa katika ujumbe. Aliposema katika luka 4:43, "*lazima nihubiri ufalme wa mbingu katika mataifa mengine, kwa maana hii ndiyo sababu niliyotumwa*"

Ili kubainisha zaidi jinsi Biblia inaelezea ufalme, tazama marejeleo haya:

1. Ufalme wa Mungu una waumini wa mataifa yote (ufunuo 5:9-10; mathayo 8:11)
2. Ufalme wa Mungu unaingiwa kwa imani ya kitoto (mathayo 18:3)
3. Ufalme wa Mungu unadhamini unyenyekevu (mathayo 18:4)
4. Ufalme wa Mungu unatenda kazi kulingana na nguvu za Mungu (1wakorintho 4:20)
5. Ufalme wa Mungu unapanuka (mathayo 24:14)
6. Ufalme wa Mungu ni wa milele (ufunuo 11:15)

## Sehemu yako ni ipi?

**Jje, tunajihusishaje katika mambo ya ufalme a Mungu?**

Ufalme wa Mungu untambulika vyema mbinguni na unaendelea kukua hapa duniani.- kwa sababu Mungu amethibiti ufalme wake kupitia watu wake. Watu wapya huingia katika ufalme wa Mungu kwa imani katika Kristo-ufalme unakua. Kanisa inapochukua injili mpembeni mwa dunia-ufalme unakua. Wakati waumini binafsi wanaishi kama chumvi katika nuru katika jamii zao, kazini na marafiki- uwepo wa Mungu unapenya sehemu hiyo n aufalme unakua.

Kuna njia kadhaa muhimu za kujihusisha katika mambo ya ufalme wa Mungu.

1. Tazamia kumjua Mungu na umwombe aishi kupitia wewe
2. Jihusishe kwa kushiriki injili, kuwakuza wafuasi, na kupeleka ujumbe wa Kristo katika mataifa (mathayo 28:19-20)
3. Ombea upanuzi wa ufalme wa Mungu
4. Kuwa sehemu ya safari fupi za misheni
5. Kuwa sehemu ya kanisa
6. Toa wakati wako, vipaji katika mambo ya ufalme
7. Ishi kama chumvi na nuru ambapo Mungu alikuweka(mathayo 5:13-16)

**Ufalme wa Mungu ni mambo yenye enzi ya Mungu ambao unaleta watu katika uhusiano ulio sawa na Mungu.**

# SEHEMU YA 14: *Ninapaswa kufanya nini na mambo niliyojifunza?*

## *Wazo kuu:*
### Unapaswa kuwakabidhi engine yale Mungu amekukabidhia.

**Muhtasari:**

- **Injili ni habari njema ya Mungu ambayo unaokoa na kumsafisha mtu. Huwezi kukua kuzidi injili.**
- **Ukristo unahusu uhusiano**
- **lengo kuu ni kumjua Mungu kwa kushiriki muda pamoja na Mungu**
- **Kushiriki wakati na Mungu kunapaswa kutiwa motisha na upendo.**
- **Maandiko ni amri ya mwisho kwa imani zote, na matendo.**
- **Maombi ni mazungussmzo pamoja na Mungu; tunanena na kusikiliza.**
- **Mfuasi ni zaidi ya muumini aliyeelimika; mfuasi anataka kuwa kama Kristo.**
- **Kumfuata Kristo ni kuwa kama Kristo**
- **Wafuasi hukuzwa wakari amababo watu wanafuata Kristo kwa kumpenda Mungu, kuungana na waumini, kuutumikia ulimwengu na kuithamini injili.**
- **kitambulizi chako kipya kinapatikana katika Kristo**
- **Jinsi ulivyompokea Kristo ndivyo utakavyotembea ndani ya Kristo**
- **Sehemu ya ukuaji wako katika Kristo inatendeka tu katika jamii**
- **Ufalme wa Mungu ni mambo yenye enzi ya Mungu ambao unaleta watu katika uhusiano ulio sawa na Mung.**

Somo lifuatalo ni mathayo 28:16-20. Linaitwa Tume Kuu. Yanatendeka tu kabla ya Yesu kupaa mbinguni. Anatoa amri moja ya mwisho kwa wafuasi wake.

*"lakini wafuasi 11 walielekea Galileo, katika mlima ambao Yesu alitua. Walpomwona, walimwabudu; lakini baadhi yao walikuwa na shaka. Naye alikuja kwao akasema –nimepewa mamlaka yote hapa duniani na mbinguni. Nendeni basi mkafanye wafuasi katika mataifa yote, mkiwabatiza katika jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu mkiwafunza kuyatii niliyowaamuru; na niko nanyi kila wakati, mpaka mwisho."*

Kuna mambo manne yanayojitokeza katika andiko hili.

1. **Wafuasi wa Yesi walikuwa na shaka.** Hata baada ya kila walichopitia na kuona mwanzo- baadhi walikuwa na shaka. Usiwe mgumu sana kwako wakati ambapo unapambana na ukweli mgumu. Usingoje hadi wakati ambapo maswali yako yamejibiwa yote kabla ya kushiriki pamoja na wenzako. Shiriki wakati ambapo unajifunza.
2. **Wafuasi huitwa kuenda.** Hatuitwi tu ili kukusanyika na kujadiliana; pia tunahitajika kutawanyika na kukuza wafuasi.
3. **Wafuasi hutii yale ambayo Kristo aliamuru.** Yesu alisema *"mkiwafunza kutii yote niliyowaamuru."* Kutii kunamaanisha kufuata kwa kina. Wafausi sio wale wanaojua ukweli wa Kristo; wafuasi ni wale wanaotii na kufuata ukweli a Kristo. Wanatenda kupitia yale wanayojua.
4. **Wafuasi hukabidhi nira ya KRISTO KWA WENGINE.** Yesu anatuambia kwa wazi *tuwakuze wafuasi katika mataifa yote...kuwafunza kutii yote niliyowaamuru*. Tunapaswa kuwakabidhi wengine mambo ambayo Kristo ametukabidhi.

**Kukabidhi ni kumpa mtu jukumu kwa jamboo Fulani**. Ikiwa tutawafunza watu kutii yale ambayo Kristo ameamuru, wako na jukumu la kuishi kulingana na mambo wanayojua.

Yuda 1:3 inasema, "*wapenzi, nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu.*" Imani ianyumiwa kwa upana kwa mafunzo ya Injili au Kristo.

Akinena na Warumi, Paulo alisema, "*shukrani kwa Mungu kwamba, hata ungawa mkikuwa watumwa wa dhambi, kwa moyo wote, mlitii mafunzo* ***mliyokabidhiwa.***" (Warumi 6:17) mafunzo ya pekee yanayowakubali watumwa wa dhambi kutii kwa moto wote ni Injili ya Kristo.

Paulo alisema katika Wagalatia 2:7, *(nilikuwa nimekabithiwa na kazi ya kuhubiri injili kwa wasioathiriwa, kama vile Petero, kwa walioathiriwa)*. Paulo alipewa jukumu la kupeleka Injili kwa wasioathiriwa, kama vile Petero, kwa walioathiriwa. Wote walikabidhiwa ujumbe wa injili.

Kwa wale walio Thesalonika, Paulo alisema, "*tunanena kama watu walioiddhinishwa na Mungu ili* ***kukabidhiwa*** *injili*" (1wathesalonike 2:4)

Alimwambia Timotheo kwamba "*mambo ambayo umesikia kutoka kwanhu katika uwepo wa mashahidi* ***yakabidhi*** *haya kwa watu waaminifu watakaowafunza wengine pia*" (2 Timotheo 2:2)

**Unapaswa kuwakabidhi watu wengine mambo ambayo Mungu amekukabidhi.**

**Madokezo ya mazoezi:**

- Anza na watu unaowajua (mf, familia , marafiki- wafanyikazi wenzako, majirani)
- Shiriki unavyoendelea kujifunza. usingoje hadi "utakapofika" ili kuanza kushiriki ukiyojifunza. Anza kukabidhi uliyojifunza sasa.
- Sio kazi yako kuwafanya watu kuamini; unapaswa kushiriki mambo uliyojifunza, kuona na kupitia na uwache Roho wa Mungu kuwaita watu mwenyewe. (matendo 1:8)
- Elekeza watu kupitia ujumbe ulio katika nakala hii
- Usijaribu kubadilisha ulimwengu katika usiku kucha. Ombea fursa na ushiriki Mungu anapoleta njiani pako.

**Andika chini majina yanayokuja akilini mwako punde:**

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________